# Maswali

1. Wakati wa Nuhu, watu gani waliishi duniani?
2. Watu wazuri walikuwa wangapi wakati huo?
3. Mungu aliamua kwangamizaje wale watu waovu?
4. Mungu alimwambia Nuhu kujenga nini, na mbona iwe kubwa?
5. Kila aina ya wanyama ngapi Nuhu aliingiza kwa Safina?
6. Mvua ilinyesha kwa muda gani?
7. Nuhu aliishi kwa Safina kwa muda gani?
8. Watu wangapi waliokoka?
9. Mungu aliahidi nini baadaye?
10. Ni ishara gani Mungu aliweka angani?


# Majibu

1. Watu waovu waliishi duniani.
2. Alikuwa Nuhu na familia yake pekee.
3. Mungu aliamua kuharibu watu waovu kwa gharika.
4. Nuhu alijenga Safina (mashua kubwa), ilikuwa kubwa ili itosheleze familia yake, wanyama wengi na ndege.
5. Nuhu alichukuwa wanyama wawili na wengine saba kila aina.
6. Ilinyesha kwa muda wa siku 40 mchana na usiku.
7. Nuhu aliishi mwaka mmoja kwa Safina.
8. Watu wanane waliokoka.
9. Mungu aliahidi kwamba hataharibu dunia kwa gharika.
10. Ishara ya Mungu ilikuwa upindi wa mvua.

**SHULE YA JUMAPILI YA CBM**

**Awamu ya 1    Mwaka wa 1**

# 4 Nuhu



## Marejeo

Mwanzo 6 – 9

## Kiini cha somo

Kuonyesha vile Mungu ana huruma na anaokoa wale wanaomwamini.

## Maneno maalum

1. Watu wengi + Waovu + Nuhu.
2. Haribu + gharika + Nuhu aokoka + Jenga + Mashua.
3. Nuhu + Onya watu + chekelea
4. Safina ikamalizika + wawili wawili + Nuhu na familia + Mungu akafunga mlango.
5. Siku arobaini (siku 40) + mvua + funika nchi + mwaka moja.
6. Safina ikatua + kunguru na njiwa + Nuhu na familia + wanyama + toka nje
7. Shukuru + ahadi + upindi wa mvua

**4.1** Somo hili kuhusu Nuhu lilitukia takribani miaka elfu baada ya kipindi ambacho Sethi alipozaliwa kwa Adamu na Hawa. Watu walimsahau Mungu. Walikuwa waovu sana. Kwa kweli, watu wakawa waovu mno hata akaghairi kwa nini aliwaumba wanadamu. Mungu akaazimu kuwaagamiza watu wote waovu kwa gharika kuu. Mungu alitazama pote duniani, akaiona jamaa moja tu iliyompendeza. Nuhu na jamaa yake walikuwa ni wenye haki na kumpenda Mungu.

**4.2** Mungu akamwambia Nuhu ya kwamba atapeleka mafuriko ya maji kuwaharibu watu wote. Mungu alimwambia Nuhu kujenga safina mkubwa. Nuhu na jamaa yake watakuwa salama ndani ya safina. Mungu alimwambia kikamilifu jinsi safina inavyopaswa kuwa. Safina ilikuwa na vyumba 3 kwenda juu kwake na kugawanywa. Pia ilikuwa na mlango na dirisha. Nuhu alimwamini Mungu na kumtii kikamilifu. Nuhu na wanawe walifanya kazi kwa bidii sana kwa miaka mingi kujenga safina. Walitumia vifaa vya mawe au mifupa na labda chuma.

**4.3** Nuhu akawaonya watu ya kwamba Mungu atatuma gharika kubwa kuiharibu nchi. Nuhu akawaambia watu watubu na kuanza kumwabudu Mungu. Lakini watu hawakumsikiliza Nuhu. Watu walimcheka Nuhu kwa kuwa alikuwa akijenga mtumbwi mkubwa, mbali na bahari. Bali Nuhu akaendelea kufanya kazi ngumu ya kujenga safina. Alimtumaini Mungu na kutii maagizo yake.

**4.4** Mwishowe Safina ikakamilika. Mungu akapeleka kila aina ya mnyama kwa Nuhu - mume na mke. Mungu akapeleka wanyama wawezao kuliwa kati ya wote saba. Wanyama wote wakaingia katika safina. Nuhu alichukua chakula kwa ajili ya wanyama wote. Ndipo Nuhu, mke wake, wanawe na wake zao wakaingia katika safina - watu wanane. Nuhu alikuwa na umri wa miaka 600 alipoingia katika safina. Nuhu na familia yake walipokuwa salama katika safina Mungu akafunga mlango.

**4.5** Nuhu na familia yake walipokuwa salama katika safina, Mungu alipeleka gharika kubwa katika dunia. Mvua ikanyesha, bahari ikapanuka na kuanza kuimeza nchi kavu, mito ikafurika. Watu waliokuwa nje ya safina wakashikwa na hofu sana. Kukawa na maji pote. Wakasema kwamba heri kama wangemsikiliza Nuhu! Lakini ilikuwa walichelewa mno! Muda sio mrefu watu wote walikufa. Mvua ilinyesha usiku na mchana muda wa siku arobaini. Kimo cha maji kikaongezeka hata maji yakaifunika nchi yote; hata vilele vya milima vilifunikwa. Kwa muda wa mwaka mmoja na siku kumi Nuhu alikuwa katika safina kwa kuwa ilichukuwa miezi 11 ili maji yakauke.

**4.6** Baada ya miezi 5 safina ikatua juu ya baadhi ya milima mirefu iliyoitwa Ararati. Baada ya miezi mingine mitatu, Nuhu aliweza kuona vilele vya milima. Nuhu alisubiri siku nyingine 40. Ndipo Nuhu akamtoa ndege aliyeitwa kunguru. Naye pia aliruka kurudi akiwa amebeba mizoga ya kula. Baadaye Nuhu alimtoa njiwa, lakini alirudi katika safina. Baadaye tena Nuhu alimtoa njiwa. Mara hii alirudi na kitawi cha mti wa mzeituni. Wakati huo Nuhu alijua ya kwamba maji yalipunguka. Nuhu na familia yake na wanyama wote wakatoka nje ya safina. Waliishi katika giza la safina kwa muda zaidi ya mwaka. Walitoka nje kuja katika ulimwengu mpya mgeni. Watu wote na kila kitu walichojua kilikwisha potea. Nuhu na jamaa yake tu waliachwa kuanza maisha mapya.

**4.7** Nuhu akamshukuru Mungu kwa kumwokoa toka katika gharika. Nuhu akajenga madhabahu na kutoa sadaka ya kumshukuru Mungu. Alimtukuza Mungu kwa kumwokoa yeye na jamaa yake. Mungu akambariki Nuhu na familia yake. Mungu aliwaambia wazae watoto wengi, ili kuianzisha jamii mpya ya watu, kumpenda na kumwabudu Mungu. Mungu akampa Nuhu ahadi rasmi. Mungu akaahidi ya kwamba hataiharibu tena dunia kwa gharika. Mungu akaweka upindi mzuri wa mvua angani, ikiwa ni ishara ya ahadi hii. Popote tukiona upindi wa mvua, tunaweza kukumbuka ahadi ya Mungu.